# ANNA OLOISHURO

## Asimulia namna safari za Ulaya zilivyompa maarifa ya kupigania ardhi kwa wanawake



**Na WARIOBA LIGOMBE**

KWA mujibu wa kitabu cha Hali ya Uchumi cha Taifa mwaka 2018, kilichotolewa Juni, mwaka huu na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) idadi ya watu Tanzania, inakadiliwa kuwa milioni 54.19 ikilinganishwa na watu milioni 52.55 mwaka 2017.

Wanawake wanadadiriwa kuwa milioni 27.68 sawa na asilimia 51.1 ya watu wote na wanaume milioni 26.51 sawa na asilimia 48.9.

Pia wanawake wamekuwa sehemu ya tegemeo la Taifa, katika mapambano ya kuondokana na umasikini kwa kushiriki shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Kilimo kinabeba idadi kubwa ya wanawake asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima na wanawake ndiyo idadi kubwa wakiwakilisha wakulima wadogo, wanaolima mazao ya chakula na biashara.

Ardhi ni rasilimali muhumu sana katika maisha ya wanawake hasa wa maeneo ya vijijini, lakini sehemu kubwa ya ardhi hususani vijijini bado inamilikiwa zaidi na wanaume huku wanawake wakikosa maeneo.

Sheria ya Ardhi za Mwaka 1999 zinabainisha haki ya mwanamke kupata, kumiliki, kutumia na kuuza au kuigawa ardhi kama ilivyo kwa wanaume maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini.

Hata hivyo zipo changamoto nyingi kwa wanawake kumiliki ardhi kwa shughuli mbalimbali zikiwemo zinazohusu kilimo na ufugaji ambapo kwa baadhi ya makabila yamekuwa yakiendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Baadhi ya jamii kutokana na mila, tamaduni ama desturi zao, zimekuwa zikichangia kuwanyima wanawake fursa ya kumiliki ardhi jambo ambalo halileti tija katika muktadha wa maendeleo ya nchi.

Anna Oloishuro mshindi wa 2016 wa Shindano la Mama Shujaa wa Chakula linaloendeshwa na Shirika la Oxfam Tanzania kupitia kampeni ya 'Grow' anasema alikuwa miongoni mwa wanawake waliopata changamoto za kumiliki ardhi.

Oloishuro anayetokea Kijiji cha Paraquyo kilichopo mkoani Morogoro anasema kuwa alipata changamoto ya kumiliki ardhi wakati akiwa kwa mume wake licha ya wanawake kuwa kuwa nguvu kazi kubwa katika shughuli za kimaendeleo nchini.



Anasema licha ya wanawake wengi kuwa nguvu kazi kubwa katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo lakini bado wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi katika umiliki wa ardhi huku wanaume wakiwa wamiliki wakuu.

"Ikitokea mama amefukuzwa au kuachana na mumewe ataondoka ingawa naye anapaswa amiliki sehemu ya ardhi ya mume wake lakini wengi hushindwa kufanya hivyo kutokana na baadhi ya jamii kutumia mfumo dume,"anasema Oloishuro.

Anasema wakati anaishi na mume wake alishindwa kumiliki sehemu ya ardhi ingawa alitumia kwa kilimo na ufugaji na kwamba baada ya kutengana alisaidiwa na ndugu zake ili aweze kupata sehemu ya kuishi.

Anasema kuwa hakukata tamaa alisimama kama mwanamke na kujishughulisha na kilimo, ufugaji na kuweza kumiliki sehemu ya ardhi kuendesha familia jambo ambalo linahitaji ujasiri wa kukabiliana nalo.

Anasema baada ya kushinda shindano hilo, shirika la Oxfam Tanzania lilimpa kifaa cha kutengeneza umeme kwa kutumia nishati ya jua iliyoanza kubadilisha maisha yake.

Anasema safari za Marekani,Uturuki na Afrika Kusini, Kenya na Ethiopia alizowezeshwa na Oxfam baada ya ushindi wake zilizidi kumfungulia milango kimaarifa na kupata nguzu zaidi katika kujikwamua kiuchumi.

"Nimepata elimu ya kujitambua na kushawishi, lakini zaidi nilifurahi nilipopewa fursa ya kuwa Jaji katika shindano la Mama Shujaa wa Chakula," anasema.

Mratibu wa Jinsia na Vuguvugu la Maendeleo ya Wanawake na Wanaume kutoka shirika la Oxfam Tanzania anasema ardhi ndiyo mtaji wa kwanza kwa mwanamke katika sula zima la kijiingizia kipato ambacho husaidia kutunza familia aliyonayo.

Mratibu huyo anaongeza kuwa, wanawake pia wanapaswa kuwa na maamzi yanayohusu matumizi ya ardhi ambapo amezitaka jamii ambazo tamaduni zao hazimpi kipaumbele mwanamke kuachana na hilo kwani nao wana haki.

Anasema kuzingatia matumizi ya ardhi ya kwa wanawake Oxfam Tanzania imekuwa ikichukua hatua za makusudi katika siyo tu kuhakikisha wanawake wanamiliki rsilimali,bali pia limekuwa liliwawezesha kujitambua.

Fatuma Gowelo mkazi wa Morogoro anaeleza adha anayokutana nayo yeye na ndugu zake baada ya kufiwa na wazazi wao ambapo anasema baba zao wadogo walijitokeza na kudai mali likiwemo shamba lenye ukubwa wa hekari 10.

Anasema baada ya vifo vya wazazi wao baba zao wadogo walijitokeza na kutaka shamba liuzwe ili wagawane fedha ambapo uamuzi wa kuuza ulifanikiwa na kuwaacha bila sehemu ya kulima

Kwa upande wake Joyce Joseph mkazi wa mkoa huo, anasema wanawake wengi katika jamii wamekuwa wakidhurumiwa ardhi na kuwaacha masikini, hivyo amewaomba wadau na serikali kuwapa elimu.

Joyce anasema wanawake ni mhimili katika jamii, lakini kutokana na changamoto wanazopata zimekuwa zikichangia juhudi zao za kujenga uchumi kukwama hivyo juhudi binafsi zinahitajika ili kuwakomboa.

Anasema mwaka 2014 alinyang'anywa shamba lake alikokuwa akimikiki tangu mwaka 1990 na alipambana ili kuhakikisha anapata haki yake lakini juhudi zake ziligonga mwamba kutokana na kukosa mtu wa kumsaidia kupata haki.

Cathbert Tomitho ni Mkurugenzi Mtendaji wa HAKIARDHI anasema taasisi yake ilianzishwa mwaka 1994 kwa lengo la kutafiti, kuibua na kuendeleza mijadala mbalimbali inayohusu haki za ardhi za wazalishaji wadodo nchini.

Anasama Sera na Sheria hii imeeleza kuwa makundi yote nchini ni haki yao kupata na kutumia ikiwa ni pamoja na kunufaika na rasilimali mbalimbali kama vile ardhi hususani kundi la wanawake ambao ndiyo tegemeo.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara 24(1) inaseleza kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, kuwa na haki ya kuhifadhi mali yake kwa mujibu wa sheria zilizipo nchini.

Kutokana na ibara hii ya Katiba ni wazi kuwa wanawake wana haki sawa ya kumiliki ardhi kisheria kama vile wanaume walivyo na haki hiyo japokuwa jamii nyingi huwaona hawastahili kumiliki ardhi.

Ili kuhakikisha changamoto ya wanawake kunyimwa fursa ya kumiliki ardhi pamoja na kutoshirikishwa kwenye maamzi yanayohusu ardhi Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) imeamua kumkomboa mwanamke.

Taasisi hiyo imeamua kumkomboa mwanamke katika jamii kwa kutoa elimu ya kisheria juu ya haki za ardhi maeneo mbalimbali nchini kwa lengo kuielimisha jamii.